TANGAZO LA SERIKALI Na. 998 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA MISITU,

(SURA YA 323)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 23(1))*

NOTISI YA KUSUDIO LA KUTANGAZA ENEO LA MSITU WA SARAME KUWA MSITU WA HIFADHI WA TAIFA SARAME YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kusudio la Kutangaza Eneo la Msitu wa Sarame kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sarame ya Mwaka 2024.

Eneo linalopendekezwa kutangazwa

**2**. Eneo la msitu ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sarame.

Madhumuni ya tangazo

**3**. Madhumuni ya kupendekezwa kutangaza Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sarame ni-

(a) kulinda eneo lililo hatarini la misitu, nyasi na ardhi oevu ambalo linatambulika kwa thamani yake ya juu ya baioanuwai, lenye upekee wa mimea na wanyama, ikijumuisha aina za mimea na wanyama walio hatarini kutoweka; na

(b) kulinda eneo la msitu na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu katika eneo la msitu huo.

Uhalali wa Notisi

**4**.-(1) Notisi hii itakuwa halali kwa muda wa siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

(2) ) Ndani ya kipindi hicho cha siku tisini, mtu au kundi la watu au mwakilishi wao anaweza, kwa maandishi kuwasilisha pingamizi, maoni au madai ya haki yoyote inayotokana na sheria za kimila kuhusiana na ardhi au mazao ya msitu au haki yoyote iliyoainishwa kwenye sheria

nyingine katika eneo ambalo linapendekezwa kutangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sarame.

Uwasilishaji wa pingamizi

**5**. Pingamizi, maoni au madai yoyote dhidi ya kusudio la kutangaza eneo la Msitu Sarame kuwa Msitu wa Hifadhi wa Taifa Sarame, yawasilishwe ndani ya siku tisini kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii katika Gazeti la Serikali kwa anuani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maliasili na Utalii,
S.L.P. 1351,
DODOMA.

*Tangazo la Serikali Na.998 (Linaendelea.)*

———

JEDWALI

———


*(Limetengenezwa chini ya aya* ya 2)

WILAYA YA BABATI

MSITU WA HIFADHI WA TAIFA SARAME

Makadirio ya eneo: Hekta 621.95 au Kilometa za Mraba 6.23

Unakopatikana na Mipaka:
Eneo lote la hifadhi awali chini ya Eneo la Msitu Sarame unaopatikana Wilaya ya Babati katika Mkoa wa Manyara kama lilivyochorwa katika Ramani Na. Jb 3081 (Skeli 1:20,000) iliyohifadhiwa na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani na lenye mipaka ifuatayo:




Dodoma,
11 Novemba, 2024

PINDI HAZARA CHANA,
*Waziri wa Maliasili na Utalii*